TATHMINI YA MADARASA YA JUU YA DISTINCTION

GREDI YA TANO - 2021
SHUGHULI ZA KISWAHILI

5

005

Jina: .....Shule .....

MAJARIBIO YA MUHULA WA PILI

Maagizo
Jibu maswali yote kulingana na maagizo.

Sehemu	A	B	C	D	Jumla
Alama	15	30	15	20	80
Upeo					

A. KUSOMA KWA SAUTI (ALAMA 15)

1. **Msomee mwalimu wako jozi za maneno zifutazo. (alama 5)**
   a) sasa, saza b) thamani, dhamana c) fuja, vuja
   d) landa, randa e) suka, zuka
2. **Msomee mwalimu wako kifungu kifuatacho ukitamka kila neno vizuri. (alama 10)**
   Msukosuko ulizuka kuhusu urithi wa shamba lililokuwa na dhahabu. Shamba hilo lilikuwa la Mzee Athumani. Mzee huyo alikuwa mzazi bali si msasi. Hata hivyo, kunao waliodhani kuwa alikuwa msasi. Wengine nao wakasema kwamba alikuwa mbadhirifu, angefuja mali yote iwapo angeachiwa. Mzee huyo alithibitisha kuwa alitaka kuwadhamini watoto walioshindwa kulipa karo katika kijiji chao. Watoto waliorandaranda walichukuliwa halahala na kufikishwa shuleni. Wengine walikuwa kama waliofufuka kutoka katika shimo la uvivu. Walisoma kwa bidii za mchwa ajengaye kichuguu kwa mate. Kutokea hapo, msukosuko huo ulitulia kabisa.

B. MASWALI MSETO (ALAMA 30)

1. Tegua kitendawili. Likienda hulia, likirudi halilii. _____ **(alama 1)**
2. Panga maneno yafuatayo jinsi yanavyofuatana katika kamusi. **(alama 1)**
   cheza, mbuzi, mama, chama _____
3. Andika majina ya sehemu zozote mbili za tarakilishi unazozijua. **(alama 2)**
   a) _____ b) _____
4. Andika maamkuzi yoyote ambayo hutumika wakati wa asubuhi. **(alama 1)**
   _____
5. Andika maagano yoyote ambayo hutumika wakati watu wanapoenda kulala. **(alama 1)**
   _____
6. Chagua nahau ya usafi. **changa bia, piga deki, ambua riziki (alama 1)**
7. Jaza jedwali ifuatalo kwa usahihi. **(alama 4)**

Kutenda	Kutendea	Kutendwa
_____	somea	_____
Cheza	_____	_____

8. Andika mifano miwili ya nomino za pekee. **(alama 2)**
   a) _____ b) _____

Distinction Educational Publishers 2021